


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA
KIBALI CHA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA NA UANGALIZI WAKATI WA
UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA ISMANI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA NA UDIWANI KATIKA
KATA 12 ZA TANZANIA BARA**

Morogoro, 01 Mei, 2026

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kanuni ya 22(4) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 01 Mei, 2026 imetoa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Kata 12 za Tanzania Bara kwa taasisi na asasi za kiraia tatu (03).

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 85(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, kikisomwa pamoja na kanuni ya 13(4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 imetoa kibali cha waangalizi wa uchaguzi kwa taasisi na asasi za ndani ya nchi mbili (02) kwa uchaguzi mdogo tajwa.

Tume inatumia nafasi hii kuzipongeza taasisi na asasi za kiraia ambazo zimepata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na kuwa waangalizi wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Kata 12 za Tanzania Bara.

Imetolewa na:


Juma I. Rahisi



KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI